



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**UFAFANUZI WA MKUTANO WA KUKUSANYA MAONI YA WADAU KUHUSU VIWANGO  
PENDEKEZWA VYA NAULI ZA ABIRIA KWA TRENI YA SGR**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilipokea maombi ya viwango vya nauli vinyavyopendekezwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuhusu nauli za treni za abiria kwa njia za Reli ya Kisasa – ‘Standard Gauge Railway’ (**SGR**) kwa ajili ya huduma ya usafiri wa treni za abiria zinazotarajia kuanza kutoa huduma mwakani 2023.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria Na. 3 ya LATRA, 2019 Mamlaka inapaswa kukusanya maoni ya wadau kabla ya kufikia uamuzi wa kuridhia viwango vya nauli kwa huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka ikiwemo nauli za treni.

LATRA, imepewa wajibu unaoelezwa katika kifungu cha sita (6)(c) na (e) cha Sheria ya LATRA kuwa ina wajibu, katika utendaji wa kazi zake, kuhakikisha kuwa inakuza ustawi wa jamii ya watanzania kwa:

- Kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma hasa katika gharama za usafiri na ubora wa huduma.
- Kuendeleza na kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa watumiaji wote pamoja na wenye kipato cha chini, watu wa vijijini na makundi maalum

Ufafanuzi huu ni kufuatia taarifa za upotoshaji zilizosambazwa mitandaoni zikiashiria kuwa nauli zinazoonekana katika tangazo la kuitisha mkutano wa wadau ndiyo nauli halisi zitakazotumika.

Taarifa hizo ni za upotoshaji, tunapenda Watanzania wafahamu kuwa LATRA haijatangaza nauli hizo, isipokuwa katika tangazo la Mkutano wa Wadau imenkuu nauli zilizopendekezwa na TRC ili wadau, ikiwa ni pamoja na watumia huduma, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC) na wananchi wote watoe maoni yao na kisha wataalam wa LATRA wachambue hoja zote kisha waandae viwango vya nauli zitakazotumika na TRC kwa treni za abiria za SGR.

Ikumbukwe kuwa LATRA imekuwa ikidhibiti viwango vya nauli kwa Treni za abiria kwa reli ya kat, mabasi ya masafa marefu na daladala kote nchini kwa ufanisi. Ufanisi huohuo utaendelea kwa nauli hizi za SGR.

Aidha, maoni ya wadau yanaweza kutumwa kwa barua pepe kupitia anuani hizi: [info@latra.go.tz](mailto:info@latra.go.tz) na [dq@latra.go.tz](mailto:dq@latra.go.tz) hadi tarehe 3 Januari 2023.

**Salum S. Pazzi**

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**

**09 Disemba, 2022**